JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI VIJANA AJIRA NA WENYE ULEMAVU



## 1.0 UTANGULIZI

- Vijana ni kundi linalochangia kwa kiwango kikubwa katika nguvu kazi ya Taifa. Takwimu zinaonyesha kuwa kwa mujibu wa sensa ya Watu na makazi ya mwaka 2012, idadi ya vijana ilikuwa 15,587,621 ambayo ni takribani 34.7% ya idadi ya watu wote,
- miongoni mwake 8,272,505 (35.9%) ni wasichana na 7,314,111 (33.4%) ni wavulana.
- kwa mujibu wa Utafiti wa Nguvu Kazi (Intergrated Labour Force Survey ) wa mwaka 2014, nguvu kazi ya vijana ilikuwa 68% ya Nguvu Kazi yote ya nchi.Hivyo vijana wanao umuhimu mkubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi

## 2.0 HATUA ZA UUNDAJI BARAZA LA VIJANA LA TAIFA

- Bunge la jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha sheria ya Baraza la vijana la Taifa Na. 12 ya Mwaka 2015.
- Kanuni za sheria ya Baraza la Vijana Tanzania zimekamilika na kutangazwa kwenye gazeti la serikali na 348 la tarehe 15 Septemba, 2017.
- Sehemu ya tano ya Kanuni imeainisha utaratibu wa kuunda kamati ya usimamizi wa uchaguzi ambayo itaratibu na kusimamia masuala yote ya chaguzi katika Baraza.

## 3.0 MUUNDO, UANACHAMA NA KAZI ZA BARAZA

(a) Muundo wa Baraza

Muundo wa Baraza la Vijana la Taifa upo katika ngazi tano ambazo ni:

i. Baraza la Vijana la Taifa

ii. Baraza la Vijana la Mkoa

iii. Baraza la Vijana la Wilaya

iv. Baraza la Vijana la Kata na;

v. Sekretarieti

Rais wa Nchi Dr Pombe Joseph Magufuli akipokea Mwenge kwenye kilele cha Mbio za Mwenge Zanzibar 2017



## 3.1 MUUNDO, UANACHAMA NA KAZI ZA BARAZA......

| NGAZI | WAJUMBE NA IDADI YAO |
| --- | --- |
| BARAZA LA VIJANA LA TAIFA | Jumla ya wajumbe 29 ambao ni: Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watakao chaguliwa na Mkutano Mkuu<br>❖ Vijana 26 (mmoja kutoka kila Mkoa) wanaowakilisha Baraza la Vijana la Mkoa<br>❖ Katibu Mtendaji |
| BARAZA LA VIJANA LA MKOA | Jumla ya wajumbe wasiozidi 50 ambao ni: Mwenyekiti<br>❖ Wajumbe 8 wa Kamati ya vijana mkoa; na<br>❖ Vijana thelathini watakaowakilisha Baraza la Vijana la Wilaya. |

## 3.2 MUUNDO, UANACHAMA NA KAZI ZA BARAZA……

| NGAZI | WAJUMBE NA IDADI YAO |
|---|---|
| **BARAZA LA VIJANA LA WILAYA** | Jumla ya wajumbe 39 ambao ni:□ Mwenyekiti<br>❖ Wajumbe 8 wa Kamati ya vijana Wilaya na:<br>❖ Wawakilishi 30 wa Vijana wenye sifa katika Wilaya husika |
| **BARAZA LA VIJANA LA KATA** | Jumla ya wajumbe wasiozidi 25 ambao ni:□ Mwenyekiti;<br>❖ Wajumbe 8 wa Kamati ya Vijana ya Kata; na<br>❖ Wawakilishi 15 kutoka kwenye vijana wenye sifa ndani ya Kata. |

## (B) UANACHAMA WA BARAZA

Kwa mujibu wa Sheria hii kifungu cha 4(3) uanachama wa Baraza utakuwa wazi na wa hiari kwa wafuataao:

i.vijana kutoka kata husika;

ii. Asasi za vijana zilizosajiliwa kwa mujibu wa Sheria

iii. vijana waliochaguliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kwa mujibu wa Sheria hii

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Mh. Jenista Mhagama mwenye dhamana ya kuwaendeleza vijana nchini**



## (C) KAZI ZA BARAZA

Sehemu ya pili ya Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa pia imeanisha kazi za Baraza kama ifuatavyo:

**(d)Majukumu Mahsusi ya Baraza Ngazi ya Mkoa, Wilaya na Kata**

| NA | NGAZI YA BARAZA | MAJUKUMU |
|---|---|---|
| 1 | **BARAZA LA VIJANA MKOA** | ❖ Kuishauri Sekretarieti ya Mkoa juu ya masuala yanayohusu maendeleo ya vijana katika ngazi ya Mkoa.<br>❖ Kuwapendekeza vijana wawili kwa ajili ya kuteuliwa kushiriki Mkutano Mkuu wa Baraza.<br>❖ Kuunda Kamati ya Vijana ya Mkoa, na<br>❖ Kufanya shughuli nyinginezo kama itakavyo elekezwa na Baraza |

## (C) KAZI ZA BARAZA.............

| NA | NGAZI YA BARAZA | MAJUKUMU |
|---|---|---|
| 2 | **BARAZA LA VIJANA WILAYA** | ❖ Kuishauri Halmashauri juu ya masuala yanayohusu maendeleo ya vijana katika ngazi ya Wilaya.<br>❖ Kuwachagua wajumbe wa Kamati ya Vijana ya Wilaya.<br>❖ Kufanya shughuli nyinginezo kama itakavyo elekezwa na Baraza |
| 3 | **BARAZA LA VIJANA LA KATA** | ❖ Kutekeleza mipango, mikakati na program za Baraza ngazi ya Kata<br>❖ Kufanya shughuli nyinginezo kama itakavyo elekezwa na Baraza |
| 4 | **SEKRETARIETI** | ❖ Kutekeleza shughuli za kila siku za Baraza |

## 4.0 TARATIBU ZA UENDESHAJI WA BARAZA

### (a) Uteuzi na Muda wa viongozi kukaa Madarakani

i.Kwa mujibu wa jedwali la kwanza la Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa utaratibu umewekwa wa muda wa viongozi kukaa madarakani; ya kwamba:

i.Mjumbe yeyote wa Baraza, mbali na mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake atakaa madarakani kwa muda usiozidi miaka mitatu kwenye masharti yatakayoainishwe kwenye hati ya uteuzi ya mjumbe huyo, lakini anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

ii. Wajumbe wa Baraza watateuliwa kwa nyakati tofauti ili muda wao wakumaliza kipindi chao umalizike kwa nyakati tofauti.

iii. Uteuzi wa viongozi wa Baraza utafanywa kwa kupitia Tangazo la Serikali.

## Vijana wa kike wahamasike katika shughuli za ujasiriamali



## (B) MIKUTANO YA BARAZA KWA MWAKA

| NGAZI | IDADI YA WAJUMBE | IDADI YA VIKAO | MAJUKUMU YA MKUTANO |
|---|---|---|---|
| **TAIFA** | 29 | 1 | ❖ Kumchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Baraza<br>❖ Kupendekeza wajumbe wa Bodi ya Ushauri<br>❖ Kuridhia mipango ya maendeleo, mikakati na programu za Baraza; na<br>❖ Kupokea, kutathmini na kuridhia utekelezaji wa mipango, mikakati na programu |

## (B)MIKUTANO YA BARAZA KWA MWAKA……..

| NGAZI | IDADI YA WAJUMBE | IDADI YA VIKAO | MAJUKUMU YA MKUTANO |
|---|---|---|---|
| **MKOA** | 50 | 2 | ❖ Kumchagua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Mkoa<br>❖ Kutekeleza mipango ya maendeleo, mikakati, na programu za Baraza katika<br>❖ ngazi ya mkoa Kupendekeza ajenda za Mkutano Mkuu na<br>❖ Kufanya kazi nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na Mkutano Mkuu |

## (B) MIKUTANO YA BARAZA KWA MWAKA……..

| NGAZI | IDADI YA WAJUMBE | IDADI YA VIKAO | MAJUKUMU YA MKUTANO |
|---|---|---|---|
| **WILAYA** | 39 | 3 | ❖ Kumchagua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Wilaya;<br>❖ Kutekeleza mipango ya maendeleo, mikakati na programu za Baraza katika ngazi ya Kata;<br>❖ Kupendekeza ajenda za Mkutano Mkuu kupitia Mkutano wa Vijana wa Mkoa; na<br>❖ Kufanya kazi nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na Mkutano Mkuu wa Baraza |

## Makamu wa Rais Mh. Samia Suluhu akifungua Baraza la Vijana Zanzibar 2012



## (B)MIKUTANO YA BARAZA KWA MWAKA……..

| NGAZI | IDADI YA WAJUMBE | IDADI YA VIKAO | MAJUKUMU YA MKUTANO |
|---|---|---|---|
| **KATA** | 25 | Kwa mujibu wa kanuni | ❖ Kumchagua Mwenyekiti wa Vijana wa Baraza la Vijana la Kata<br>❖ Kutekeleza mipango ya maendeleo, mikakati na programu za Baraza katika ngazi ya kata; na<br>❖ Kufanya kazi nyingine yoyote kama itakayoelekezwa na Mkutano Mkuu wa Baraza. |

## 5.0 BODI YA USHAURI YA BARAZA

**(A) WAJUMBE WA BODI**

Sehemu ya nne ya Sheria ya Baraza la Vijana kifungu 21(1) inatamka kuundwa kwa

Bodi ya Ushauri ya Baraza ambayo itaundwa na wajumbe wafuatao:

i.Mwenyekiti wa Bodi atakayeteuliwa na Rais;

ii. Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Taifa;

iii. Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Vijana;

iv. Afisa sheria atakayemwakilisha Mwanasheria Mkuu; na

v. Vijana watano watakaochaguliwa na Baraza na kuridhiwa na Waziri.

## 5.1 BODI YA USHAURI YA BARAZA............

**(B) SIFA ZA MTU ANAYEFAA KUWA MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI**

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

i.Angalau ana shahada ya kwanza kutoka chuo kinachotambuliwa;

ii. Ameonesha uwezo wa uongozi kwa vijana na kuwaunganisha vijana pamoja

iii. Ana weledi katika au amechangia kikamilifu katika kuhamasisha ajenda ya maendeleo ya vijana; na

iv. Ana uaminifu wa hali ya juu, maadili na ana muitikio katika mahitaji na matarajio ya vijana

## Waziri Mkuu Mh.Kasim Majaliwa akisisitiza jambo kwa maendeleo ya Nchi



## (C) KAZI ZA BODI

Kazi kuu za Bodi zitakuwa ni:

i. Kulishauri Baraza kwa ujumla katika utekelezaji wa mamlaka na kazi zake zilizoainishwa chini ya Sheria hii.

ii. Kufanya kazi nyingine kama itakavyopewa au itakavyoelekezwa chini ya Sheria hii.

## 6.0 KAMATI ZA VIJANA ZA KATA, WILAYA, NA MIKOA

**(a) Kamati ya Vijana ya Kata**

Kamati ya vijana ya Kata itaundwa na:

i.Mwenyekiti atakayechaguliwa na Baraza la Kata kutoka miongoni mwa vijana wenye sifa ndani ya kata.

ii. Wajumbe sita watakaowakilisha vijana kutoka kwenye kata husika;

iii. Katibu atakayeteuliwa miongoni mwa vijana wenye sifa ndani ya kata

**(b) Kamati ya Vijana ya Wilaya**

- Baraza la vijana la Wilaya litaunda Kamati itakayoitwa Kamati ya Vijana ya Wilaya.

Kamati ya vijana ya Wilaya itakuwa chombo cha Baraza la Wilaya ambalo litaundwa na:-

i. Mwenyekiti atakayechaguliwa na Baraza la Wilaya kutoka miongoni mwa vijana wenye sifa ndani ya Wilaya

ii. Vijana sita watakaowakilisha vijana wenzao katika wilaya husika;

iii. Katibu atakayeteuliwa miongoni mwa vijana wenye sifa ndani ya wilaya.

**(c) Kamati ya Vijana ya Mkoa**

Kamati ya vijana ya Mkoa itaundwa na:

i.Mwenyekiti atakayechaguliwa na Baraza la Vijana la Mkoa kutoka miongoni mwa vijana wenye sifa ndani ya mkoa husika

ii. Wajumbe sita watakao wakilisha asasi za vijana zenye usajili tena zilimo ndani ya Mkoa husika

iii. Katibu atakayeteuliwa miongoni mwa vijana ndani ya mkoa

Muhimu: Mtu hataweza kuwa mjumbe wa Kamati au Baraza la Vijana la Kata, Wilaya na Mkoa isipokuwa ni mkazi wa Mkoa husika.

## Vijana wakijadiliana kuhusu Malengo Endelevu ya Dunia (SDG,s)



## 7.0 FEDHA NA MALI ZA BARAZA

Sehemu ya Tano ya Sheria ya Baraza la Vijana inahusu masharti ya fedha na kwamba imebainisha fedha za Baraza, makadirio ya mwaka na ukaguzi wa hesabu.

(a) Fedha na mali za Baraza zitajumuisha:

i. Fedha zote kama zitakavyopangiwa matumizi na Bunge kwa madhumuni ya Baraza;

ii. Fedha zote au mali zinazoweza kuingia kwenye Baraza wakati likitekeleza mamlaka yake au kutimiza wajibu wake chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote;

iii. Michango kutoka mamlaka ya serikali za mitaa;

iv. Zawadi kama zinavyoweza kutolewa kwa Baraza; na

v. Fedha zote kutoka chanzo chochote kilichotolewa, zilizochangwa au kukopeshwa kwa Baraza.

## 7.1 FEDHA NA MALI ZA BARAZA

(b) **Bajeti na matumizi ya Baraza kwa Mwaka**

- Baraza litatayarisha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka husika na kuwasilisha kwenye Bodi walau miezi 3 kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha.
- Bajeti ya mwaka itaidhinishwa na Baraza kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha unaohusika na kuridhiwa na Waziri. Baraza halitarekebisha bajeti ya mwaka bila ya idhini ya Waziri.
- Matumizi hayatofanywa kwa madhumuni ya Baraza isipokuwa kwa kuzingatia makadirio ya mwaka au kwa kuzingatia ridhaa ya Baraza iliyotolewa baada ya maandishi ya Waziri.
- Baraza, ndani ya miezi mitatu kila baada ya mwisho wa mwaka wa fedha, litawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za Baraza zinazohusu mwaka huo.

## 8.0 UTEUZI WA KAMATI YA UCHAGUZI

kwa mujibu wa kifungu Na.24 (2) cha Kanuni za sheria ya baraza la vijana la Taifa kimebainisha kwamba wajumbe tisa (9) wa kamati ya usimamizi wa uchaguzi wa viongozi wa Baraza watateuliwa na Waziri anayehusika na masuala ya vijana. Uteuzi wa wajumbe hao utatokana na uwakikilishi kutoka katika taasisi za Serikali zifuatazo:-

1. Wajumbe watatu kutoka katika Wizara inayohusika na Masuala ya Vijana;
2. Mjumbe mmoja kutoka Wizara inayohusika na masuala ya Maendeleo ya Jamii, jinsia na watoto;
3. Mjumbe mmoja kutoka wizara inayohusika na masuala ya tawala za Mikoa na serikali za Mitaa(TAMISEMI);
4. Wajumbe wengine watatu wenye uelewa wa masuala ya vijana kutoka katika sekta ya umma;
5. Mjumbe mmoja kutoka Ofisi ya Mwanasheria mkuu wa serikali.

## Vijana washiriki katika shughuli za ujasiriamali



## 9.0 MAMLAKA YA KAMATI YA UCHAGUZI YA BARAZA LA VIJANA LA TAIFA

**Mamlaka (Mandate)**

Kamati ya Usimamizi wa uchaguzi ya Baraza la vijana ni chombo kilichoundwa kisheria kwa mujibu wa Kanuni namba 24 ya Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa, 2017. Kamati hii itakuwa na jukumu kisheria katika kuandaa taratibu na kusimamia shughuli zote za uchaguzi wa viongozi na wajumbe wa Baraza la Vijana la Taifa kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa.

## 10.0 **MAWANDA YA KAZI (SCOPE OF WORK)**

- Kamati ya Usimamizi wa Uchaguzi wa Baraza la vijana la Taifa ina wajibu wa kuandaa utaratibu na kusimamia shughuli zote zinayohusu masuala Uchaguzi wa Viongozi na wajumbe wa Baraza la Vijana la Taifa.

**Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa uchaguzi wa Baraza.**

- Waziri wa Mwenye Dhamana na masuala ya Vijana kwa mujibu wa Kanuni ya 24 ya Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa, atateua wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa masuala ya Uchaguzi. Uteuzi huu utazingatia mapendekezo ya wawakilishi kutoka katika Taasisi na Wizara zifuatazo:-

## 11.0 MWENYEKITI WA KAMATI

Wajumbe wa Kamati watachagua Mwenyekiti pamoja na Katibu miongoni mwao ili kusimamia na kuratibu zoezi zima la uchaguzi katika ngazi zote (Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa). Uongozi huu utadumu kwa muda wa miaka mitatu

**11.1 Majukumu ya Kamati:**

Kamati ya usimamizi wa uchaguzi wa viongozi wa Baraza la Vijana la Taifa itatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Baraza la Taifa na itakuwa na majukumu kama ifuatavyo:

(a) Kusimamia Uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Taifa, Mkoa, Wilaya na Kata isipokuwa wale walioteuliwa kwa mujibu wa nyadhifa zao;

(b) Kuhakiki Daftari la wapiga kura

(c) Kuthibitisha wagombea;

(d) Kulinda kura pamoja na maboksi ya kupigia kura

## Kilimo cha kisasa kitamkomboa kijana na umaskini wa kipato



## 12.0 UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA BARAZA LA VIJANA LA TAIFA, MKOA, WILAYA NA KATA.

Mtu yeyote mwenye nia ya kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Taifa, Mkoa, Wilaya au Kata atajaza fomu itakayotolewa na Kamati ya Baraza ya Usimamizi wa Uchaguzi kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la pili katika Kanuni hizi

Kamati ya Usimamizi wa Uchaguzi:-

(a) itachambua maombi na kuendesha usaili kwa madhumuni ya kupata majina ya watu watatu.

(b)itawasilisha majina yaliyoteuliwa chini ya aya ndogo ya (a) katika Mkutano Mkuu kwa madhumuni ya kufanya uchaguzi wa Mwenyekiti


## 13.0 UTEUZI WA KATIBU MTENDAJI WA BARAZA

- Baraza litapokea maombi kutoka kwa waombaji vijana wenye sifa ili kujaza nafasi ya Katibu Mtendaji
- Baada ya kupokea maombi chini ya kanuni ndogo ya (1), Baraza litachambua maombi hayo, kufanya usaili, kisha kuwasilisha majina ya vijana watatu kwa Waziri ambaye atamteua Katibu Mtendaji miongoni mwa majina hayo.

## 15.0 WAJUMBE WA BODI YA USHAURI YA BARAZA

- Mkutano Mkuu utapokea maombi kutoka kwa waombaji wenye sifa ambao siyo wajumbe wa Bodi ya ushauri ya Baraza la Vijana kutokana na nyadhifa zao kugombea nafasi hizo.
- Baada ya kupokea maombi chini ya kanuni ndogo ya (1), Mkutano Mkuu utayachambua na baada ya kujiridhisha utateua majina matano ya vijana kwa ajili ya idhini ya Waziri

## Vijana ndio watunzaji wakubwa wa mazingira



## 16.0 HITIMISHO

Pamoja na maeneo yaliyojadiliwa kutokana na Sheria ya uundwaji wa Baraza la Vijana masualamengine yaliyozingatiwa ni pamoja na:

(a)Wadau kuhakikisha wanawajumuisha vijana kutoka katika makundi yenye mahitaji maalum kama vile wenye ulemavu, vijana walio kwenye mazingira hatarishi na maeneo yasiyofikika na kuonekana kirahisi

(b) Kufahamu kwamba Baraza hili kwa mujibu wa Sheria hii siyo chombo cha kisiasa au jukwaa linaloendesha Kampeni za ki-chama, ki-dini wala ukabila.

(c) Baraza la Vijana ni sauti ya vijana wote nchini kwa lengo la kuhamasisha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo yao wenyewe pamoja na jamii kwa ujumla.


(d) Baraza litakuwa chombo kitakachochangia kwa kiwango kikubwa katika juhudi za kudumisha misingi ya utawala bora, uzalendo, amani, umoja na mshikamano miongoni mwa vijana pamoja na taifa kwa ujumla.

## 16.1 HITIMISHO............

(e) Baraza la Vijana la Taifa litatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na Serikali pamoja na wadau mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ili kufikia malengo ya Baraza

(f) Katika kutekeleza majukumu yake, Baraza la Vijana la Taifa litazingatia kwa kiwango kikubwa usawa wa kijinsia kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda.

(g) Baraza la Vijana la Taifa ni chombo cha Kitaifa ambacho pia kitatoa uwakilishi wa vijana kitaifa na Kimataifa. Hivyo kitafanya kazi kwa kuzingatia uzalendo, nidhamu na weledi wa hali ya juu ikiwemo kuheshimu utamaduni wa Kitanzania.



ASANTE KWA KUNISIKILIZA

